

Fomu ya Maelezo ya Kibadala cha COVID-19

Je, kibadala ni nini?

Virusi hubadilika mara kwa mara kupitia mabadiliko virusi vinaposambaa, hali inayosababisha kuwepo kwa tofauti za virusi asili vinavyojulikana kama kibadala. Vibandala ni mabadiliko madogo ikilinganishwa na toleo la asili la virusi na vinaweza kuathiri kiwango cha maambukizi na kuathiri ubaya wa ugonjwa unaosababishwa na virusi.

Je, kibadala cha Delta ni nini?

[Kibadala cha Delta](#) au aina ya B.1.617.2, iliyotambuliwa mara ya kwanza nchini India, ni kibadala kilichotajwa kuwa kibadala cha “faafu na cha kasi” cha COVID-19 kufikia leo. Sasa ni aina ya virusi vinavyotawala nchini Marekani. Kinasemekana kusambaa kwa urahisi na haraka zaidi kuliko vibadala vingine. Tafiti nyingine zinasema kuwa kibadala cha Delta pia huongeza hatari ya mtu kuwa na matokeo mabaya baada ya maambukizi ya COVID-19. Public Health England ilichapisha [utafiti](#) kutoka Scotland ukionyesha kwamba watu walioambukizwa kibadala cha Delta walikuwa na uwezekano wa zaidi ya 85% kulazwa hospitalini wakilinganishwa na wale waliombaukizwa vibadala vingine (Alpha ya juu).

La kutia wasiwasi kuhusu kibadala cha Delta ni kwamba kinaonekana kuenea kwa urahisi zaidi miongoni mwa watu wa umri wa chini. Hii inaweza kusababisha visa zaidi vya COVID-19, ongezeko la wanaolazwa hospitalini na uwezekano wa vifo zaidi. Watoto na watu wazima wa miaka 5-49 wana uwezekano wa [mara 2.5](#) zaidi kuambukizwa kibadala cha Delta wakilinganishwa na wale walio na miaka 50 au zaidi. Hali hii inaangazia umuhimu wa watu wote, si tu wale walio kwenye ongezeko la hatari, kuchanjwa. Pia inasisitiza umuhimu wa kuvalia barakoa na kudumisha umbali na watu wengine kwa wale wasioweza kupata chanjo.

Je, chanjo zinafanya kazi dhidi ya kibadala cha delta?

Utafiti wa mapema unaonyesha kuwa chanjo zilizo nchini Marekani: Pfizer, Moderna na Johnson & Johnson, zinatoa kinga dhidi ya kibadala cha Delta. Kwa upande mwingine, watu ambao hawajachanjwa kikamilifu, au wale ambao wanachanjwa awamu moja (dozi moja ya Pfizer au Moderna), wako kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa kibadala cha Delta. Taarifa za sasa kuhusu utendakazi wa chanjo ni kama zifuatazo:

- Pfizer imeripotiwa kufanya kazi 87.9% wiki mbili baada ya dozi ya pili dhidi ya kibadala cha delta; hii inalinganishwa na ufaafu wa 33.2% baada ya dozi ya kwanza. [Uchanganuzi](#) wa watu 14,019 walio na kibadala cha pia ulionyesha kuna ufaafu wa 94% dhidi ya ugonjwa mbaya (yaani, kulazwa hospitalini) baada ya dozi moja na 96% baada ya dozi mbili.
- Chanjo ya Moderna ni sawa na Pfizer na inatarajiwa kufanya kazi inayolingana.
- Data kamili ya ufaafu duniani bado haipatikani kwa chanjo ya Johnson & Johnson COVID-19. Hata hivyo, Johnson & Johnson imetoa [taarifa](#) kuhusu ufaafu kulingana na mazingira ya

maabara. Waliangalia sampuli za damu kutoka kwa wagonjwa wanane na kupata chanjo yao ina upunguaji mdogo katika kusawazisha kingamwili lakini bado inakinga dhidi ya kabadala cha Delta.

Je, kwa nini ni muhimu kuchanjwa?

Tangu mwanzo wa janga la COVID-19, desturi za usalama kama vile kupima, kujitenga, kuvaa barakoa na kudumisha umbali na wengine zimefanya kazi ili kupunguza kasi ya msambao wa virusi. Ingawa desturi hizi zinaendelea kuwa muhimu, chanjo ni kinga bora dhidi ya COVID-19. Huku vijana wakiwa kwenye ongezeko la hatari na watoto chini ya miaka 12 kutoweza kuchanjwa, ni muhimu kwa wale wanaoweza kuchanjwa kufanya hivyo haraka iwezekanavyo. Watu ambao hawajachanjwa na hawawezi kuchanjwa wanapendekezwa kuvalia barakoa na kudumisha umbali katika maeneo ya umma. Kwa kuchanjwa hujikingi wewe tu bali jamii yako. Pia unatekeleza wajibu muhimu wa kukomesha COVID-19 kubadilika na kuwa vidadala vingine thabiti na hatari zaidi.

Je, ninahitaji kuchanjwa ikiwa awali nilikuwa na COVID-19?

Kingamaradhi baada ya [maambukizi ya awali](#) huwalinda watu dhidi ya maambukizi kwa hali nyingine. Hata hivyo, [kingamaradhi](#) hutofautiana pakubwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Pia haijulikani muda ambao kingamaradhi inadumu kutokana na maambukizi ya asili au jinsi itakavyofaulu dhidi ya vidadala vipya. Watu waliokuwa na ugonjwa wa COVID-19 awali wanapendekezwa kuchanjwa. Kutokana na uwezekano wa COVID-19 kusababisha matokeo mabaya ya afya na kwa sababu unaweza kupata maambukizi tena, kila mtu anapaswa kuchanjwa bila kujali maambukizi ya awali ya COVID-19. Watu wanaweza kuamua kusubiri siku 90 kati ya maambukizi na chanjo. Pia kuna kipindi cha kusubiri kinachopendekezwa kwa wale waliopata COVID-19 na kupata tiba ya kingamwili ya kloni moja.

Je, ninaweza kupata wapi chanjo ya COVID-19?

Taarifa kuhusu watoa huduma wa chanjo ya COVID-19 na kliniki karibu nawe zinaweza kupatikana kwenye ukurasa wetu wa [Chanjo ya COVID Vaccine Locator](#). Watu binafsi wanaweza pia kuwasiliana na NDDoH Hotline kwa 1.866.207.2880 kwa usaidizi wa kuratibu miadi ya chanjo.